Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 01 Issue: 01 | April -2019
www.editoncpublishing.org
*Mwangi, J. Ndung'u., et al., Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Ulinganishi wa Matatizo Ya Kijamii Yanayowakumba Majagina Katika Tendi Za Mikidadi Na Mayasa Na Kalevala

**Jackson Ndung'u Mwangi[1]; Prof. Wendo Nabea[2]; Dkt. Sheila Wandera[3]**

**Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu**
**Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya**
**Corresp. Author E-mail: jigmwas@gmail.com**

**IKISIRI**

Uwepo wa tendi katika maeneo ya Afrika umezua mjadala na mgogoro mkali mno katika jamii ya usomi. Hii ni kutokana na rai kuwa wasomi na watafiti wengi kutoka maeneo ya Kimagharibi walidai kuwa Afrika hakuna tendi ila kinachodaiwa kuitwa tendi ni masimulizi ya kisifo tu. Wahakiki wengine wamezifutilia mbali tendi hizi kwa kudai kuwa maudhui yake ni ya kichawi na sihiri. Pia, vigezo vya kuainisha tendi vilivyotumiwa na wanazuo wa Kimagharibi vilikuwa vya kimaeneo na kimakusudi, walidhalilisha tendi za Kiafrika. Licha ya kuwa kuliibuka watafiti wa Kiafrika na kudai kuwa Afrika kuna tendi, wao pia walielekea kutumia vigezo ambavyo ni vya kimaeneo. Ili kujaribu kutatua mzozo na utata uliopo kuhusu uwepo wa tendi katika maeneo ya Kiafrika, utafiti huu ulinuia kuchunguza iwapo kuna uwiano wa matatizo ya kijamii yanayowakumba majagina baina ya tendi za maeneo haya mawili. Madhumuni makuu yalikuwa kutathmini iwapo kuna uwiano wa matatizo ya kijamii yanayowakumba majagina baina ya tendi za Kiafrika na zile za Kimagharibi licha ya tendi za Kiafrika kufutiliwa mbali na baadhi ya wasomi wa Kimagharibi. Mtafiti alinua kutafiti tendi mbili ambazo ni *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* unaopatikana Afrika na *Utendi wa Kalevala* unaopatikana Finland katika maeneo ya Kimagharibi. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa iliyoasisiwa Joseph Campbell (1987). Utafiti huu ni wa muundo wa kiudhamano na mahali pa utafiti palikuwa ni katika Maktaba. Inatarajiwa kuwa utafiti huu utakuwa mchango mkubwa kwa jamii ya wasomi hasa wanaoshughulikia fasihi linganishi na utajaribu kutatua ubishi ulioko kuhusu tendi za maeneo mbalimbali.

**Maneno ya kimsingi:** Majagina, utendi, matatizo ya kijamii, motifu

-------------------------------------------------------------------***-------------------------------------------------------------------

***How to cite this article in APA (6th Edition):***

Mwangi, J.N., Nabea, W., & Wandera, S. (2019). Ulinganishi wa matatizo ya kijamii yanayowakumba majagina katika tendi za mikidadi na mayasa na kalevala. *Editon Cons. J. Kiswahili.*, 1(1), 14-21.

-------------------------------------------------------------------***-------------------------------------------------------------------



**© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org**

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 01 Issue: 01 | April -2019
www.editoncpublishing.org
*Mwangi, J. Ndung'u., et al., Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**Utangulizi**

Tendi nyingi za Kiswahili huwa na wahusika wakuu ambao ni mashujaa na ambayo hudhaminiwa sana katika jamii kutokana na matendo yao ya kikepee yenye umuhimu katika jamii. Licha ya kuwa mashujaa hawa huwa na sifa za kipekee na wengine wao hutenda matendo ya kiungu, ni dhahiri huwa pia wao hukumbana na matatizo ya kijamii ambayo humkumba mwanadamu wa kawaida. Kemunto (2015) anachangia suala hili kwa kudai kuwa mashujaa katika tendi huwa na matatizo chungu nzima wakiwa katika ari ya kutimiza jaala zao. Alidokeza kuwa mashujaa hawa wanakumbana na matatizo na vikwazo vingi ambavyo ni sharti wazue mikakati na mbinu kabambe za kuepuka matatizo haya. Baadhi ya matatizo haya ni kama vile, kusalitiwa na wanajamii, kukumbana na vita vikali, kuogopwa na wanajamii pamoja na kutembea safari ndefu sana huku wakikumbana na njaa isiyo kuwa na kifani.

Ouma (2013) pia alichangia suala hili na kudokeza kuwa shujaa katika tendi hukumbwa na matatizo chungu nzima. Anadai kuwa takribani majagina wote katika tendi hukumbana na matatizo mengi sana na viunzi anuwai ambavyo lazima wajaribu kuviepuka ili waafikie jaala zao. Anadai kuwa, licha ya kuwa Nabii Isa alikuwa na sifa nyingi za Kiungu na matendo yake yalikuwa ya kimiujiza na Kiungu, alikumbana na shida nyingi ambazo humkumba mwanadamu yeyote yule wa kawaida. Kwa mujibu wa watafiti hawa, imebainika wazi kuwa ni kweli majagina katika tendi hukumbwa na matatizo chungu nzima ya kijamii.

**Mwega wa nadharia**

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa. Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa iliasiwa na Joseph Campbell (1904- 1987) na kuhakikiwa na wanafalsafa wengine wa fasihi na soshiolojia kama vile Rank (1999) na Timothy Lynns (2009). Joseph Campbell alidokeza kuwa ili shujaa katika tendi aweze kuafikia jaala yake, lazima apitie hatua mbalimbali zitakazomwezesha kuafikia azma ile. Campbell alidokeza misingi mitatu katika nadharia hii.

Kwanza, ni kuondoka kwa shujaa. Katika kitengo hiki, Campbell anadokeza kuwa ni sharti shujaa aondoke katika taifa lake na aiache jamii yake. Msingi wa pili ni kufundwa na kushindwa kwa shujaa. Katika kitengo hiki, shujaa hupatana na mambo kadha wa kadha. Shujaa hujitenga na kuishi peke yake pale katika makazi ya kipekee kama vile jangwani. Akiwa pale, hukumbana na adui ambaye hupigana naye vita vikali.

Mhimili wa tatu ni kurejea na kurudi nyumbani kwa shujaa. Baada ya kushindwa na maadui pamoja na mahasidi wake, shujaa huamua kurejea nyumbani ili aweze kuungana na wanajamii wake. Anaporudi nyumbani, hukumbana na adui mwingine na vita vingine vikali huzuka pale ambapo wakati mwingi jagina huyu huibuka kuwa mshindi.

**Matatizo yanayowakumba mashujaa katika tendi**

Katika tendi za Kiswahili, Shujaa hukumbana na matatizo chungu nzima ambayo kwa kawaida humkumba mwanadamu wa kawaida. Licha ya kuwa shujaa ana sifa za kiungu, yeye pia anaweza kukumbana na matatizo chungu nzima ya kijamii kama vile kutengwa na wanajamii, kupatwa na njaa pamoja na kiu, kusafiri safari ndefu zilizojaa hatari,



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 01 Issue: 01 | April -2019
www.editoncpublishing.org
*Mwangi, J. Ndung'u., et al., Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kuhadaiwa, kuogopwa na wanajamii, kujawa na uoga, matatizo katika ndoa pamoja na kupatwa na upweke.

**Kuhadaiwa**

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, inabainika wa kuwa mashujaa katika utendi huu wanahadiwa na wanajamii hususan na watu wa jamii zao za karibu. Majagina Mikidadi na Mayasa wanadhihirika kama mashujaa wakuu wanaotenda matendo ya kipekee katika jamii zao. Mikidadi anapopigana na Mayasa na kumpiku katika vita, inabainika wazi kuwa hata yeye ni shujaa kutokana na weledi anaoudhihirisha katika vita. Jambo hili linawafanya wawili hawa kuamua kuoana. Jabiri anajaribu kuwahadaa majagina hawa ili wasioane kwa kumwekea Mikidadi kiwango kikubwa cha mahari ili ashindwe kulipa. Pia, Jabiri anajaribu kumhadaa Mikidadi kwa kukataa kumpa pete baada ya maelewano yao. Jabiri anatumia mbinu hizi ili Mikidadi ashindwe kumuoa binti huyu, jambo ambalo lingemfanya amwoze Mayasa mume mwingine mwenye mali nyingi.

Katika *Utendi wa Kalevala*, suala la shujaa kuhadaiwa pia linadhihirika na kuathiri azimio la jaala yake kwa kiwango kikubwa. Baada ya Yokahani kujibizana na kumdunisha shujaa Mwanamwini, Mwanamwini anamfanyia sihiri ambayo inamfanya kuteseka na kuathirika sana. Anajipata akiwa ziwani huku nguvu za sihiri zikimtosa majini polepole. Alipokuwa karibu kuzama majini kabisa na kuangamia, Yokahani anamwahidi Mwanamwini kuwa akimwacha huru, atamwoza dadake aitwaye Aino kama inavyodhihirika katika ukurasa wa 26. Hii ni hadaa tu kwani Yokahani hata hakuwa amezungumza na dadake kuhusu suala hili. Mwanamwini anapokutana na Aino mwituni akitafuta kuni, Aino anakataa katakata uhusiano wowote na Mwanamwini na anapopewa pete, shanga na nguo za dhamana kubwa, anazikataa na kuzitupa mchangani. Matukio haya yanadhihirisha waziwazi kuwa Mwanamwini alihadaiwa na Yokahani na pia Aino.

**Kupatwa na njaa au kiu**

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, shujaa pia anakumbana na hali ya kupata njaa pamoja na kiu kisichokuwa na kifani. Baada ya Mikidadi kuwekewa kiwango kikubwa cha mahari na Jabiri, anafunga safari akiwa na mtumwa wake aitwaye Khamisi kwenda jangwani kutafuta mali ya kulipia ile posa. Katika ubeti wa 169, inadokezwa kuwa wawili hawa walichoka sana baada ya kusafiri safari ndefu kwa siku nane. Pia, inadaiwa kuwa walipatwa na kiu na njaa kali mno hadi wakashindwa kusafiri na afya kuathirika sana.

*Siku ya nane kipita, Mikidadi atoshele,*
*Chakula hapana hata , Hawezi kwenenda nbele,*
*Maji hayapati kata, Kwa kiu imzidie,*
*Haya yaliyosalia. Mtumwawe kamwambia.*
*Ubeti wa 169 Ubeti 170.*

Beti hizi zinaonyesha kuwa ijapokuwa Mikidadi alikuwa shujaa wa kutambulika, alipatwa na njaa pamoja na kiu kama mwanadamu wa kawaida.

Katika *Utendi wa Kalevala*, suala la shujaa kupatwa na njaa linaonekana kushamiri mno. Mwanamwini kama shujaa alisafiri safari ndefu hadi akafika mojawapo ya nchi katika Kalevala iitwayo Pelawini. Akiwa pale, alipatwa na njaa kupita kiasi na akaamua kutafuta kuni ili apike chakula. Akiwa katika harakati za kutafuta kifaa cha kukatia kuni, anapatana na Samsa, aliyejulikana kwa jina la kimajazi kama mkata miti.



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

ISSN: 2663-9289

Volume: 01 Issue: 01 | April -2019
www.editoncpublishing.org
*Mwangi, J. Ndung'u., et al., Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Katika harakati ya kumtafutia Mwanamwini kuni, Samsa anaukata mti wa kipekee uitwao Sindiani, uliokuwa na umuhimu wa kipekee katika tamaduni za watu wa Kalevala. Ukataji wa mti huu baadaye unasababisha kiangazi katika nchi hii na kusabaisha njaa kubwa mno inayomwadhiri hata Mwanamwini. Isitoshe, Mwanamwini alipokuwa akiishi nchi ya Vainola alipatwa na njaa kali mno, jambo lililofanya afya yake kuathirika vibaya sana. Mifano hii inadhihirisha wazi kuwa hata shujaa wa kutajika kama Mwanamwini hupatwa na njaa licha ya kuwa aliaminika kuwa na sifa za kipekee na za kiungu.

**Kusafiri safari ndefu mno**

Akizungumzia kuhusu suala la safari katika tendi, Timothy (2010) alidokeza kuwa kwa kweli shujaa katika tendi hujihusisha na safari chungu nzima akiwa katika azma ya kuafikia jaala yake. Alidokeza kuwa safari hizi huwa na umuhimu wa kipekee kwani hukuza sifa tabia na kuibua dhamira mbalimbali katika tendi zenyewe. Alitambua kuwa shujaa anapojihusisha na safari hizi, baadhi yazo huwa ngumu sana na hata wakati mwingine huathiri afya zao. Vile vile, safari hizi hukumbwa na vizingiti anuwai ambavyo huathiri maisha ya shujaa.

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, inabainika wazi kuwa mashujaa walisafiri safari ndefu ambayo iliwachosha mno na hata kuathiri afya zao. Katika Ubeti wa 169, inadhihirika fika kuwa Mikidadi alisafiri safari ndefu mno akiwa na mtumwa wake Khamisi kuelekea jangwani kutafuta mahari ya kumlipia Mayasa. Alisafiri usiku na mchana bila kupumzika jambo lililomfanya kupatwa na njaa isiyokuwa na kifani. Safari hii ina umuhimu wa kipekee katika utendi huu kwani inamwandaa Mikidadi kuwa mtahimilivu katika azimio lake la kuafikia jaala zake.

Katika *Utendi wa Kalevala*, ukurasa wa 21, inabainika kuwa mashujaa katika jamii hii walikumbwa na tatizo la kusafiri safari ndefu. Katika uchanganuzi wa tendi, safari huwa ni kipengele muhimu kwa maisha ya shujaa katika kuafikia jaala yake. Katika ukurasa huu wa 21, Yokahani anaonekana akisafiri safari ndefu mno kumtafuta Mwanamwini ili aweze kupigana naye na kudhihirisha ushujaa wake. Inadokezwa kuwa alimchukua farasi wake na kumpeleka mbio sana huku akipita juu ya saruji, safari iliyomchukua siku nyingi kuikamilisha. Baadaye Yokahani alionekana kuchoka zaidi na afya yake ilidhoofika na kuathirika sana kutokana na safari hii ndefu.

**Kuogopwa na kutengwa na wanajamii**

Kwa mujibu wa Michaux (2003), shujaa katika tendi hukumbwa na matatizo anuwai katika jamii. Akitafiti kuhusu changamoto zinazobainika kwa shujaa katika tendi za *Gilgamesh* na *Homer,* alitambua kuwa mashujaa hawa walikumbwa na matatizo chungu nzima kama vile kutengwa na jamii, kujawa na upweke na kuhadaiwa na wanajamii. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa shujaa kwa kweli hukumbana na matatizo chungu nzima. Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, mashujaa wanaonekana kuogopwa na wanajamii, jambo ambalo linatinga utangamano na ushirikiano na wanajamii wenzao. Kutokana na urembo wa Mayasa, inadaiwa kuwa wanaume waliokuwa matajiri na wenye kutajika walisafiri safari ndefu kutoka maeneo tofautitofauti ili waweze kumuoa Mayasa. Walipofika nyumbani, Mayasa anadai kuwa yule atakayemuoa ni sharti wapatane katika vita na atakayemshinda ndiye atakayemuoa. Katika ubeti



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 01 Issue: 01 | April -2019
www.editoncpublishing.org
*Mwangi, J. Ndung'u., et al., Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

wa 60, inadokezwa kuwa Mayasa kama shujaa aliwapiga na kuwauwa wanaume wengi na wengine wengi walimkimbia kwa ajili ya kumuogopa.

*Hawale wataka ndoa,*
*Ikawa kupinduliwa,*
*Mayasa akiwaua,*
*Wengi wakamkimbia,*
*Ubeti 60*

Inabainika wazi kuwa kwa kweli, mashujaa katika jamii hii waliogopwa kutokana na matendo yao ya kuogofya na kutisha. Jambo hili lilitinga uhusiano wao na wanajamii. Kutengwa huku kunadhihirika pale ambapo hata Mayasa hatangamani vyema na wazazi wake kwani wao pia wanamuogopa hata kujadiliana naye kuhusu maswali ya kimsingi ya kindoa. Katika ubeti wa 66 hadi 73, Mamake Mikidadi (Tamima) anaonekana kumuogopa Mayasa kutokana na matendo yake ya kuogofya. Anamkanya na kumkataza Mikidadi kwenda kupigana na Mayasa kwani alihofia kuwa pengine angepoteza maisha yake katika vita.

Katika *Utendi wa Kalevala*, mashujaa pia wanaonekana wakitengwa na wanajamii, jambo linaloathiri pakubwa azimio lao la kuafikia jaala zao. Baada ya Yokahani kumwahidi Mwanamwini kuwa angemwoza dadake Aino, Aino anaonekana kumwogopa sana Mwanamwini kutokana na matendo yake ya kuogofya na ya kutisha katika jamii. Aino anaonekana kusononeka, kulia na kuudhika mno alipoambiwa kuwa angeoana na Mwanamwini. Aino hakupenda shujaa huyu kwani alikuwa na sifa za kuogofya, alikuwa mzee zaidi aliyejawa na mvi kichwani na alikuwa na umaarufu wa kutumia sihiri iliyowaathiri na kuwatesa watu. Suala hili linadhihirika katika ukurasa wa 26 pale ambapo Mwanamwini anakutana ana kwa ana na Aino akiwa mwituni akitafuta kuni. Anapompa Aino pete ya kipekee, shanga za dhahabu na mavazi ya bei ghari, Aino anazitupa chini na kumtokora huku akilia kwa kumwogopa. Vile vile, wazazi wake Yokahani walimwonya asiende kukabiliana na Mwanamwini kwani ni shujaa wa kuogopwa kutokana na uwezo wake wa kipekee wa kutumia sihiri. Sifa hizi za shujaa kuogopwa katika jamii kuliwafanya watengewe na jamii.

**Matatizo katika ndoa**

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, mashujaa wanaonekana kuwa na matatizo chungu nzima wakiwa katika azma ya kufunga ndoa yao. Kwanza, baada ya Mikidadi kukabiliana na Mayasa na kumshinda katika ndoa, familia ya Mayasa ikiongozwa na Jabiri haikufurahishwa na hali hii na inatumia njia zotezote zile kujaribu kupinga ndoa hii. Jabiri anamwekea Mikidadi kiwango kikubwa cha mahari ili ashindwe kulipa. Alijaribu kutumia hila ili Mikidadi aogope na afutilie mbali azimio lake au ashindwe kulipa ili baadaye amuoze Mayasa mume mwingine mwenye mali. Pili, ndoa ya Mikidadi na Mayasa ilikumbwa na matatizo kwani Jabiri alitaka kutumia hila kwa vile hakutaka kumpa Mikidadi pete baada ya maelewano yake na Mayasa. Mikidadi anaelevuka na kuitisha pete ile kabla ya kwenda kutafuta mahari. Akiwa jangwani kuitafuta mahari, azimio la ndoa yake linakejeriwa. Luhani anamdhihaki na kumwambia kuwa yeye ni mume aliye maskini na Mayasa alimkataa kutokana na hali ya umaskini aliyo nayo. Haya yanadhihirika katika ubeti wa 227 na 228.

*Luhani akatongoa, Ukasiri ua watu,*
*Khabarizo nazijua, Masultani wenzetu,*
*Ati ukitaka ndoa, Kwa ndoa isiyo na kitu,*



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

ISSN: 2663-9289

Volume: 01 Issue: 01 | April -2019
www.editoncpublishing.org
*Mwangi, J. Ndung'u., et al., Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

*Mke akaukataa. Hutamanije kuoa.*

*Ubeti 227*
*Ubeti 228*

Katika *Utendi wa Kalevala*, mashujaa wanaonekana kukumbwa na matatizo katika ndoa. Kwanza kabisa, Mwanamwini anakataliwa na Aino aliyeahidiwa kumuoa. Suala hili linamwathiri sana Mwanamwini kama shujaa na kumwacha akiwa na huzuni na upweke usiokuwa na kifani. Mwanamwini akiwa safarini kutoka Vainola kuelekea nchi ya Pohiola, anakaribishwa na Malkia wa nchi ile aitwaye Luohi. Luohi anampa makaribisho ya kifalme na kumpa chakula cha kipekee. Malkia Luohi alikuwa na binti mrembo kupindukia na wa kutajika aliyependeka kwa wengi. Mwanamwini anataka kumuoa binti huyu lakini anamkataa na kudai kuwa yeye anataraji kuoana na mwanamume shujaa aliye na uwezo wa kutengeneza na kutumia kifaa kiitwacha sampo. Jambo hili linamuudhi sana Mwanamwini na kumwacha akiwa na upweke na huzuni isiokuwa na kifani.

**Upweke.**

Katika *Utendi wa Kalevala*, suala la shujaa kujawa na upweke linajitokeza. Inadaiwa kuwa Shujaa Mwanamwini akiwa Vainola, hakuwa na marafiki ila aliishi peke yake katika kisiwa cha Vainola huku akitunga nyimbo na kujiimbia. Hii ni kutokana na hali kuwa alikuwa katika nchi geni na hakuwa na rafiki yeyote ambaye angeshirikiana naye au hata kufanya urafiki. Haya yanadhihirika katika ukurasa wa 20.

*Akakaa Mwanamwini, Vainola masikani,*
*Kisiwa cha Vainola ndio nchi Kalevala,*
*Nyimbo zake akighani, ghinaya bila kifani,*
*Laila na naharia, nyimbo akijiimbia,*
*Huzuni kimjazia, na upweke sio kifani.*

*Ukurasa 20.*

Ubeti huu unadhihirisha wazi kuwa kwa kweli, Mwanamwini alikuwa na upweke mwingi sana kwani hakuwa na watu wa kutangamana nao.

Katika nchi ya Kalevala, inadhihirika wazi kuwa nchi hii ilikuwa na mashujaa chungu nzima na kila shujaa alikuwa na umuhimu wake katika jamii. Mmoja wa shujaa hawa aliitwa Yokahani na alipenda vita na umaarufu sana. Baada ya kupata fununu kuwa Mwanamwini alikuwa Vainola, alifunga safari kwenda kukabiliana naye kwani alikuwa na kinyongo kutokana na umaarufu wa Mwanamwini kama mtunzi mashuhuri wa nyimbo na mashairi. Anapopatana na Mwanamwini, Mwanamwini anadhihirisha upweke aliokuwa nao katika ukurasa wa 22.

*Mwanamwini mwenye siri, kajibu na kukariri,*
*"Mimi siwi mashuhuri, wala siwi mafuri,*
*Sifahanu usihiri, wala sijui shairi.*
*Ninakaa peke yangu, ni mbali na ulimwengu,*
*Kati kwangu mashambani, nasikia wangu nyuni.*

*Ukurasa 22.*

Katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, mashujaa pia wanapatwa na upweke mwingi unaoathiri maisha yao sana. Baada ya Mikidadi kwenda jangwani kutafuta mahari ili waoane na Mayasa, inamchukua wakati mwingi mno kwani aliwekewa kiwango kikubwa mno cha mahari. Inadaiwa kuwa wakati mwingi, Mikidadi alipatwa na upweke mwingi huku akiwa na mawazo chungu nzima kuhusiana na hali ya bibiye Mayasa. Kwa upande mwingine, Mayasa pia alipatwa na upweke usiokuwa na kifani baada ya Mikidadi kuchukua muda kurudi nyumbani. Alihofia sana maisha ya Mikidadi akiwa kule jangwani. Pia, upweke unamzidia Mayasa wakati inadaiwa kuwa angeozwa



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

mume mwingine baada ya Mikidadi kukawia kurejea nyumbani. Ni wazi kuwa licha ya kuwa wawili hawa walikuwa mashujaa, wanakumbana na matatizo ya kijamii yanayowapata wanajamii wa kawaida. Pia, imebainika kuwa mashujaa katika *Utendi wa Kalevala* na *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* wanakumbana na matatizo sawa ya kijamii yanayowapata wanajamii wa kawaida licha ya kuwa wao ni majagina wenye sifa za kiungu.

**Mapendekezo na hitimisho**.

Kwa mujibu wa utafiti huu, imebainika wazi kuwa kuna uwezekano wa kazi za maeneo mbalimbali ya kijiografia kuathiriana na kuingiliana katika viwango mbalimbali. Licha ya kuwa baadhi ya wasomi na wanazuo wa Kimagharibi walifutilia mbali uwepo wa tendi katika maeneo ya Kiafrika, utafiti huu umebaini kuwa kwa kweli, majagina katika tendi za maeneo haya mawili wana sifa za kishujaa zinazowiana na kuingiliana. Pia, majagina hawa wanakumbwa na matatizo sawa ya kijamii yanayowakumba wanajamii wa kawaida. Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa mashujaa katika tendi huwa na umuhimu wa kipekee katika jamii zao na hukumbana na pingamizi chungu nzima katika azimio la kuafikia jaala zao. Imebainika kuwa mashujaa katika tendi za maeneo haya mawili wanahadaiwa, wanapatwa na njaa, wanatengwa na wanajamii wao, wanasafiri safari ndefu, wanapatwa na matatizo katika ndoa zao na pia wanajawa na upweke maishani mwao.

Tunapendekeza kuwa tafiti za baadaye zishughulikie suala la dini katika tendi na pia zishughulikie suala la nafasi ya mwanamke kwa shujaa katika tendi.

## Marejeleo

Campbell, J. (1949). *The Hero with Thousand Faces.* New World Library: Novato.

Deme, M. K. (2009). *Heroism and the Supernatural in the African Epics towards a Critical Analysis.* Western Michigan University.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Clarendon: Oxford University Press.

Heinman (1972). *Utendi wa Mikidadi na Mayasa.* Nairobi: East Africa publishers Limited,

Lynns, T. (2009). *New Perspectives in Campbells Mononyth Theory*. New Jersey: Princeton University press.

Mulokozi, M. M (1997). *Utendi wa Nyakiiru Kibi*. Tanzania: ECOL publication Morogoro

Njogu, K., & Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Kifasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

**Tasnifu**

Kemunto, J. (2015). *Uhakiki Linganishi wa Sifa za Mashujaa: Sakawa na Fumo Liyongo*. University of Nairobi. M.A Thesis.



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

ISSN: 2663-9289

Volume: 01 Issue: 01 | April -2019
www.editoncpublishing.org
*Mwangi, J. Ndung'u., et al., Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Michaux, G. (2003). *Gilgamesh and Homer: a Comparative Study of Motifs Sets, Distinctions and Similarities*. Open Universitet. Antwerpen. M.A. Thesis.

Ouma, O. K. (2013). *Uhakiki wa Maudhui Teule Katika Utenzi wa Nabii Isa*. University of Nairobi. M.A. Thesis.

Timothy, P.J.P. (2010). *The Exile in Homeric Epics*. University of Toronto. PhD thesis.



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org